MKUTANO WA TANO WA BARAZA LA TAIFA LA BIASHARA ULIOFANYIKA TAREHE 4 DESEMBA 2008, KUNDUCHI BEACH HOTEL & RESORT

1.0 **WALIOHUDHURIA**

Tafadhali angalia Jedwali na. 1

2.0 **UFUNGUZI**

2.1 Bwana Phillemon L. Luhanjo, Mwenyekiti wa Kamati ya Utendaji ya Baraza la Taifa la Biashara, aliwakaribisha wajumbe na washiriki mbalimbali na kutambua kuwepo kwa Mheshimiwa Mwinyi Haji Makame, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Zanzíbar, Mheshimiwa Dkt Mary Nagu (Mb), Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko na Bibi Esther Mkwizu, Mwenyekiti Mwenza wa Kamati ya Utendaji ya Baraza la Biashara la Taifa.

Bwana Luhanjo alieleza kuwa wajumbe waliohudhuria mdahalo huo walichaguliwa kutokana na nyadhifa, nafasi na ujuzi wao binafsi.

2.2 Bwana Luhanjo alieleza kwamba maudhui ya mkutano ni mdahalo wa kitaifa wa uwezeshaji wananchi kiuchumi na aliwashukuru na kuwapongeza watayarishaji wa mdahalo huo ambao ni Baraza la Taifa la Biashara (TNBC) na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC).

2.3 Bwana Luhanjo alimkaribisha Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania na Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Biashara afungue Mkutano.

3.0 **DONDOO ZA HOTUBA YA UFUNGUZI WA MKUTANO YA MHESHIMIWA JAKAYA MRISHO KIKWETE, RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA NA MWENYEKITI WA BARAZA LA TAIFA LA BIASHARA**

3.1 Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe na washiriki mbalimbali kwenye mdahalo. Pia alitambua ushiriki wa wajumbe wa Baraza la Taifa la Biashara, Uongozi wa Mabaraza ya Biashara ya Mikoa, Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Wajumbe wa Kikundi Kazi cha Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

3.2 Mwenyekiti alikumbusha kwamba Serikali imetekeleza sera mbalimbali za kuwawezesha wananchi kiuchumi tangu kupata uhuru mwaka 1961. Sera hizo ni pamoja na 'Africanisation', Azimio la Arusha, Vijiji vya Ujamaa, Viwanda vidogovidogo, Elimu ya Kujitegemea n.k. Mafanikio ya sera hizo yalikuwa ya mchanganyiko ambapo baadhi ya sera zilifanikiwa na nyingine zilikuwa chini ya matarajio. Serikali bado inaendelea na dhamira yake ya kuwawezesha wananchi kiuchumi kama ilivyoainishwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2000 aya ya 6.

3.3 Kupitishwa kwa Sera na Sheria ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi mwaka 2004 na uundwaji wa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi mwaka 2005 pamoja na uanzishwaji na uimarishwaji wa mifuko mbalimbali ya uwezeshaji wananchi kiuchumi ni vielelezo dhahiri vya dhamira ya Serikali ya kuwawezesha wananchi kiuchumi.

3.4 Mwenyekiti alisisitiza kuwa mdahalo ulenge katika kueleza dhana nzima ya uwezeshaji wananchi kiuchumi ikizingatiwa kuwa Serikali peke yake haiwezi ikafanikiwa kuwawezesha wananchi bila ushirikiano wa wadau kama sekta binafsi na mashirika yasiyo ya Kiserikali pamoja na mtu binafsi. Ukweli ni kwamba uwezeshaji unaanza na juhudi za mtu mwenyewe binafsi katika kutumia fursa zilizopo katika mazingira yanayomzunguka. Uelewa wa mtu binafsi na uboreshaji wa mazingira ndio njia kuu ya uwezeshaji. Fikra za utoaji wa mitaji peke yake ni dhana potofu ya uwezeshaji. Mikakati, dira na miongozo ya mdahalo ijikite katika maswali ya nini kifanyike, nani afanye na vipi uwezeshaji ufanyike.

3.5 Mwenyekiti alimalizia hotuba kwa kusisitiza kuwa uzoefu uliopatikana katika kuunda Mabaraza ya Biashara ya Mikoa usaidie kwenye kuanzisha na kuendesha Mabaraza ya Biashara ya Wilaya na hili litakuwa ni jukumu la Mabaraza ya Biashara ya Mikoa yakishirikiana na Baraza la Taifa la Biashara.

4.0 **KUPITISHWA KWA AGENDA**

Agenda ilipitishwa kama ilivyopendekezwa na Mwenyekiti.

5.0 **KUMBUKUMBU MBALIMBALI ZA BARAZA**.

Mkutano ulipokea na kuthibitisha kumbukumbu zifuatazo:

- Mkutano wa Nne wa Baraza la Taifa la Biashara uliofanyika tarehe 11 Desemba 2006.
- Ripoti za Mwaka na Hesabu za Baraza la Taifa la Biashara kwa miaka ya 2005/06 na 2006/07.

Mkutano ulipokea kumbukumbu zifuatazo:

- Mkutano wa Pili wa Wawekezaji wa Ndani (LIRT) uliofanyika tarehe 9 Februari 2007
- Mkutano wa Sita wa Wawekezaji wa Nje (IIRT) uliofanyika tarehe 10-12 Machi 2007

Maelekezo

Mwenyekiti aliagiza kuwa mikutano ijayo ya Baraza la Taifa la Biashara itoe taarifa ya utekelezaji wa maagizo yatokanayo na kumbukumbu za mikutano iliyopita.

6.0 **KUWASILISHA MADA YA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI**

6.1 **Utangulizi**

Bwana Reginald Mengi, Mwenyekiti wa Kikundi Kazi cha Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi cha Baraza la Taifa la Biashara alitoa maelezo ya utangulizi jinsi kikundi kilivyofanya kazi na kusisitiza kuwa dhamira ilikuwa kushauri mfumo wa uwezeshaji wa Kitanzania (home grown model) ambao umelenga juhudi za mtu binafsi na wananchi kwa ujumla bila kutegemea misaada kutoka nje. Pia alishauri kuwa mafanikio ya utekelezaji wa mapendekezo ya kikundi kazi unategemea sana utashi wa kisiasa (political will).

6.2 Mada ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

Mada ilitolewa na Prof. Lucian Msambichaka ikisisitiza mambo makuu yafuatayo:-

6.2.1 Chimbuko

Chimbuko la mdahalo ni Mkutano wa Nne wa Baraza la Taifa la Biashara na Mkutano wa Pili wa Wawekezaji wa Ndani ambayo kwa nyakati tofauti ilisisitiza umuhimu wa kutazama dhana nzima ya uwezeshaji wananchi kiuchumi.

6.2.2 Mchakato wa Utayarishaji

- Midahalo ilianzia ngazi ya Wilaya, Mikoa hadi mdahalo wa Kitaifa ikishirikisha wadau mbalimbali katika ngazi husika kwa ajili ya kuongeza ushiriki na umiliki wa zoezi zima.
- Wadau walitoa mawazo, changamoto na kuibua fursa zinazowazunguka kwa ajili ya utekelezaji ili kuboresha maisha yao.

6.2.3 Midahalo ya Wilaya na Mikoa

Midahalo ya Wilaya na Mikoa ilizingatia mambo yafuatayo:

- Uwezeshaji ni Nini
    - Kuwasaidia wananchi kutambua na kuongeza uwezo wao wa ubunifu na uzalishaji
    - Kutengeneza mazingira yanayofaa kwa ajili ya uwekezaji, uzalishaji na biashara.
- Nani awezeshwe
    - Wakulima, wavuvi, wafugaji na wachimbaji madini wadogo wadogo
    - Sekta isiyo rasmi na biashara ndogo sana, ndogo na za kati
    - Wataalamu,wafanyakazi wa fani mbalimbali.
    - Wafanyabiashara wa kati na wakubwa.

- Mategemeo ya Wananchi kuhusu uwezeshaji
    - Maisha yao kuwa bora zaidi

- Changamoto
    - Changamoto za uwezeshaji ni kwenye elimu, ujasiriamali, mtazamo wa jamii (mind set), sheria na tija.
- Shughuli za Uwezeshaji
    - Shughuli kubwa zinazoendelea mikoani na wilayani ni kilimo, biashara na huduma

- Mapendekezo ya mikoa kuhusu utekelezaji na uendelevu wa uwezeshaji:
    - Kuanzisha na kuendeleza mafunzo ya ujasiriamali na elimu ya kilimo na ufugaji, mikopo ya muda mrefu, mitaji na huduma za kifedha, miundombinu hasa umeme na mawasiliano, viwanda, masoko ya uhakika na taarifa za masoko.
    - Uwezeshaji uwe sehemu ya mipango ya wilaya na mikoa kwa ajili ya uendelevu, aidha ufuatiliaji na tathmini zifanyike.

6.2.4 Majumuisho na Mwelekeo wa Baadaye

Wilaya na Mikoa ilitoa maamuzi, majukumu na misimamo yao ya utekelezaji na usimamiaji wa zoezi zima la uwezeshaji ikizingatia yafuatayo;

- Kila mkoa uwe na mpango mkakati endelevu wa uwezeshaji kiuchumi

- Kuwepo dawati la uwezeshaji kutoka wizara zote husika hadi wilayani.
- Kuweko vigezo vya kupima maadili ya utendaji bora (***code of good practice***) katika serikali kuu, serikali za mitaa, wizara, idara, mashirika, wakala wa Serikali na makampuni binafsi ili kuimarisha uwazi, utawala bora na uwajibikaji
- Kufanya mabadiliko ya haraka ya sheria ili biashara ndogo ndogo zimilikiwe na Watanzania; biashara za jumla zimilikiwe na Watanzania au ziwe kwa ubia na wageni.
- Kufanyia marekebisho sheria za madini ili leseni za uchimbaji ziwe kwa Watanzania au ziwe ni kwa ubia wa Watanzania na wageni.
- Kufanyia marekebisho sheria za ardhi ili ardhi imilikiwe na Watanzania
- Serikali itoe upendeleo maalumu kwa makampuni ya Kitanzania na yale yanayosaidia uwezeshaji wa Watanzania kiuchumi hasa kwenye shughuli ya manunuzi.
- Kuharakisha kupunguza gharama za kufanya biashara (Cost of Doing Business), ngazi ya wilaya, mkoa na taifa.
- Wizara zote zishirikiane kikamilifu na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ili lifanye kazi yake kwa ufanisi.
- Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania awe Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

7.0 MAJADILIANO YA JUMLA

Majadiliano ya jumla yalisisitiza yafuatayo:

7.1 **Uwezeshaji ni nini:**

- Ni juhudi za kila mtu binafsi kujiendeleza kiuchumi kwa kutumia fursa zilizopo katika mazingira yanayomzunguka.
- Juhudi maalumu za Serikali katika utungaji sera, sheria na taratibu kwa lengo la kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara zinazowezesha wananchi kukua kiuchumi.
- Watu kutambua na kuongeza uwezo wao wa ubunifu na uzalishaji.

7.2 **Nani Awezeshe**

- Serikali kwa kutunga sera, sheria na taratibu za uboreshaji mazingira ya uwekezaji na biashara kwa madhumuni ya kuwawezesha wananchi washiriki kikamilifu katika shughuli za uchumi.
- Mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs/CBOs) yahamasishe kila mtu mwenye uwezo wa kufanya kazi afanye kazi, kurudisha utamaduni wa kufanya kazi kwa bidii, nidhamu na ufanisi na matumizi bora ya muda.
- Sekta binafsi kuunda vikundi na kongano ili kuboresha thamani na kuongeza tija katika uzalishaji na huduma. Mabenki kurahisisha masharti ya utoaji mikopo.

7.3 **Nani awezeshwe**

- Wakulima, wavuvi, wafugaji na wachimbaji madini wadogo wadogo hususani wanaoishi chini ya shilingi elfu moja kwa siku.
- Vikundi vidogo visaidiwe ili viweze kufanya biashara na Serikali
- Vyama vya ushirika vya msingi viimarishwe kwa kupewa elimu ya kutunza fedha, kuweka mahesabu, ukopeshaji na mikopo ya riba nafuu.

- Wenye shughuli katika sekta isiyo rasmi na biashara ndogo sana, ndogo na za kati.
- Wataalamu kwenye fani za kilimo, matibabu ya mifugo na binadamu, uvuvi, uhandisi, usanifu wa majengo, sheria, uhasibu n.k
- Wafanyabiashara wa kati na wakubwa.

7.4 **Mbinu za uwezeshaji**

Mbinu za uwezeshaji ziende sambamba na kuboresha mazingira ya biashara na kupunguza gharama zake.

- Ardhi kuwa chombo kikuu cha uwezeshaji wananchi kiuchumi hivyo ithamanishwe na imilikiwe na Watanzania na itumike kama dhamana ya kupatia mikopo na kuingia ubia na wawekezaji.
- Kuainisha, kuelimisha na kuhamasisha wananchi kuhusu fursa za ndani na nje ili wazitumie kwa manufaa yao na taifa.
- Kutoa elimu kwa wakulima na wajasiriamali juu ya tija, ongezeko la thamani, taratibu za biashara na ushindani wake.
- Kukuza uwekezaji kutoka ndani na nje na kuhakikisha wananchi wanafaidika na uwekezaji huo.
- Kuunda vikundi na kongano kwa ajili ya kuwawezesha wananchi kiuchumi na wilaya ziwe kama nchi na zishindane.
- Kujenga tabaka la kati ambalo litakuwa chimbuko kubwa la wajasiriamali na soko muhimu la ndani.
- Kuhakikisha na kuongeza ubora na viwango (Quality and Standards) katika uzalishaji mazao, bidhaa na utoaji huduma.
- Kutoa upendeleo maalumu kwa makampuni yanayomilikiwa na Watanzania kwenye utoaji huduma na manunuzi.
- Kuwe na mkakati maalumu wa kuongeza usindikaji wa bidhaa na mazao ghafi ili kuzalisha ajira na kuinua kipato cha Mtanzania kwa kuuza bidhaa zilizoongezewa thamani.
- Kuharakisha mchakato wa uanzishaji Benki za Maendeleo hususani Benki ya Maendeleo ya Kilimo.
- Kuhamasisha ujenzi wa viwanda vidogovidogo, vya kati na vikubwa na kukuza mahusiano ya manunuzi kati ya viwanda hivyo
- Kuimarisha Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wanachi Kiuchumi kwa kutengewa bajeti ya kutosha, ili liweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu.
    - Kamati ya Utendaji ya Baraza la Taifa la Biashara ilitambua ufinyu wa bajeti ya Serikali na kuliagiza Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi litafute vyanzo vingine vya mtaji kwa ajili ya ukopeshaji.
- Rais wa Tanzania awe Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ili kuongeza msukumo wa utekelezaji wa majukumu ya Baraza.
    - Kamati ya Utendaji ya Baraza la Taifa la Biashara ilitambua umuhimu wa kuboresha utendaji kazi wa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na kuagiza liwe chini ya Kamati ya Kiuchumi ya Baraza la Mawaziri.

- Vyombo vya habari vihamasishe wananchi kuhusu uwezeshaji

7.5 **Utekelezaji**

Serikali inaendelea kuchukua hatua kadhaa za uwezeshaji kama zifuatazo:

- Sheria ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi
    - Kutunga Sera ya Uwezeshaji (2004), Sheria yake no.16 ya 2004, kuanzishwa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (2005) na Mifuko ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.
- Credit Reference Bureau na vitambulisho
    - Ilipendekezwa kuimarishwa kwa Credit Reference Bureau sambamba na kuweka taratibu za Watanzania kuwa na vitambulisho ili, pamoja na mambo mengine, kusaidia upatikanaji wa mikopo.
- GPS – Digital Mapping
    - Ilipendekezwa digital mapping ifanyike nchi nzima, kama ilivyofanyika mikoa ya Pwani na Kilimanjaro, ili kurahisisha upatikanaji wa ardhi kwa wawekezaji.
- Hati Miliki
    - Ilipendekezwa kuboresha na kuharakisha upatikanaji na usajili wa hati miliki za ardhi ili zitumike kama dhamana ya kupatia mikopo na kuingia ubia.

8.0 UZINDUZI WA MABARAZA YA BIASHARA YA WILAYA

8.1 Utangulizi

Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Biashara, Bwana Dunstan Mrutu alieleza kuwa kutokana na mafanikio makubwa ya kuanzisha Mabaraza ya Biashara ya Mikoa, ulikuwa wakati muafaka wa kuzindua Mabaraza ya Biashara ya Wilaya, madhumuni makubwa yakiwa:

- Mabaraza ya Wilaya ni chombo cha mwanzo cha majadiliano kati ya sekta binafsi na sekta ya umma kwa lengo la kuboresha mazingira ya kufanya biashara na uwekezaji,
- Kupeleka mafanikio ya ukuaji wa uchumi mpana katika ngazi ya chini ya uchumi wa jamii kwa kuwahusisha wananchi katika majadiliano ya namna ya kuibua fursa za uwekezaji kwa ajili ya kuzalisha ajira, kukuza kipato, kuongeza tija na kuchangia katika kupunguza umaskini ngazi ya vijiji hadi wilaya.
- Mabaraza ya Biashara ya Wilaya yanaundwa ili pawe na chombo cha kuratibu, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa programu mbalimbali za maendeleo ya uchumi ya wananchi.
- Misingi ya Mabaraza ya Biashara ya Wilaya ilianzishwa wakati wa mchakato wa midahalo wa uwezeshaji wananchi kiuchumi ngazi ya Wilaya ikijumuisha wajumbe toka sekta ya umma na sekta binafsi.

8.2 Uzinduzi Rasmi wa Mabaraza ya Biashara ya Wilaya

Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Biashara, Rais Jakaya Mrisho Kikwete, alitamka rasmi kuzinduliwa kwa mabaraza ya biashara ya Wilaya zote Tanzania na kutoa maelekezo yafuatayo:

- Mabaraza ya Mikoa yakishirikiana na Baraza la Taifa la Biashara yalee Mabaraza ya Wilaya na kuhakikisha kwamba yanatimiza lengo kuu na yanafanya kazi kwa ufanisi.
- Baraza la Taifa la Biashara lipitie upya Waraka wa Rais No. 1 wa 2001 ili kuangalia muundo wake kwa kuainisha vyombo vyake yakiwemo Mabaraza ya Biashara ya Mikoa na Wilaya.

9.0 KUFUNGA MDAHALO

- Mkutano uliridhia maudhui ya mdahalo wa uwezeshaji wa wananchi kiuchumi.
- Maelekezo yalitolewa ya kutengeneza hatua za utekelezaji wa maamuzi yaliyopendekezwa kwenye mdahalo.
- Kwa ajili ya kuboresha mazingira ya biashara katika ngazi ya mkoa, zoezi la kutathmini gharama za uanzishaji na uendeshaji biashara kimkoa likamilishwe na matokeo yake yatumike kama kigezo cha kupima utendaji ngazi ya Wilaya na Mkoa.
- Mdahalo ufanyike kila mwaka ukiwa ndio wakati muafaka wa kutoa tuzo za utendaji bora katika dhana nzima ya uwezeshaji.
- Mdahalo ujao ujikite katika maswala ya gharama za kuendesha biashara kimkoa (Regional Cost of Doing Business) na ardhi.

Mwenyekiti alifunga mkutano saa 12:30 jioni kwa kuwashukuru wajumbe kwa michango na ushiriki wao mkubwa.

Mh. Jakaya Mrisho Kikwete
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
na Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Biashara